
# Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA TOLEO LA 2 2018 Bei Sh. 1,000/-



## YALIYOMO NDANI

- TOLEO MAALUM NDANI CWME
- Tofauti za udhehebu ni utajiri
- Moto wa Injili wafifia ulaya
- Walutheri wenye asili ya Afrika wakutana
- Ufuasi ni kujitolea
- Maaskofu KKKT na ELCA wakutana Uhuru Hotel

TOLEO LA 2 2018 ISSN 0856 - 1214 Na. 2 Vol. 118

# FAHAMU HISTORIA FUPI YA KKKT

## Vyama vilivyo eneza Ulutheri

Mwanzo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika (baadaye Tanzania) kuwepo nchini ni mwaka 1887, Chama cha Misioni cha 'Berlin III' au 'Evangelical Missionary Society for East Africa' (EMS) kutoka Ujerumani kilipoanzisha kazi ya Injili Kigamboni, Dar es Salaam.

## Chama cha pili

Chama cha Misioni cha 'Berlin I', nacho kutoka Ujerumani, kiliingia Tanzania kikitokea Afrika ya Kusini na kuanza kazi Nyanda za Juu Kusini mwaka 1891 kilipoanzisha kituo au misheni sehemu iitwayo Ipagika au Pipagika (Wangemannshöhe) katika Dayosisi ya Konde kwa sasa.

Mwaka 1890, Chama cha Berlin III kilichukua sura mpya baada ya kubadili sera yake na kujulikana kwa jina la Bethel au 'Misioni ya Bethel'. Misioni hii ikafika sehemu za Tanga na kuanza kazi eneo la Mbuyukenda.

Baadaye Misioni hii iliamua kufikisha Injili ya Kristo nje ya mipaka ya Tanganyika. Wamisionari hao walipanga kwenda Rwanda kupitia Bukoba. Walipofika Bukoba wakafungua kituo mwaka 1910.

## Chama cha Leipzig

Chama cha tatu kufika nchini Tanzania ni Chama cha Misioni cha Leipzig, nacho kutoka Ujerumani. Kiliingia Tanganyika mwaka 1893 na kuanza kazi ya Misioni Kaskazini mwa nchi sehemu ya Kidia, Old Moshi na baada ya muda mfupi, kwa kushauriwa na Mtawala wa Kijerumani, Carl Peters, wakahamia Nkwarungo - Machame.

Pamoja na vyama vilivyoanzisha Ulutheri Tanzania, kuna mchango mkubwa wa vyama vya Misioni na makanisa toka Ulaya na Marekani tunayo endelea kushirikiana nayo kama: COS, ELCB, FELM, DLM, DANMISSION, SEM, LMW, MEW, NLM, NMZ, BMW, UEM, VELKD, ELCA, nk. Hakika Neno la Mungu linaendelea kufundishwa kwa upendo na kwa usahihi wakati wote huu.

## Vita za Dunia

Kanisa la Kilutheri nchini lilipita katika nyakati ngumu vipindi vya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia 1914 hadi 1918 na ya Pili 1939 hadi 1945. Chama cha Misioni Augustana kutoka Marekani pamoja na Walutheri kutoka nchi nyingine za Ulaya walitoa msaada sana wakati wamisionari wa Kijerumani walipoondoka.

## Makanisa Saba

Vyama vya Misioni viliendelea na kazi ya Injili na makanisa saba ya Kilutheri yakaanzishwa maeneo mbalimbali nchini. Makanisa hayo mwaka 1948 yaliunda Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Tanganyika. Tarehe 19 Juni 1963 makanisa yale saba yaliungana kuunda Kanisa moja la **KKKT** na makanisa yakageuka kuwa Dayosisi au Sinodi. Sinodi zikageuka kuwa Dayosisi. Hivi sasa KKKT ina Dayosisi 26.

## Uongozi na usimamizi

Chombo kikuu cha maamuzi KKKT ni Mkutano Mkuu ambao hufanyika kila baada ya miaka minne. Halmashauri Kuu ya KKKT hukutana mara mbili kwa mwaka kwa vikao vyake vya kawaida. Wajumbe wa vyombo vyote hivi wanawakilisha Dayosisi zote za KKKT.

## Kazi za Umoja

Kanisa lina vituo na Ofisi Kuu ya Kazi za Umoja (Common Work). Ofisi Kuu ya Kanisa inaongozwa na Katibu Mkuu. Ina idara zifuatazo: Misioni na Uinjilisti; Mipango na Maendeleo; Fedha na Utawala; Huduma za Jamii, Kazi za Wanawake na Watoto. Pia kuna Kitengo cha Ukaguzi. Kazi ya Ofisi Kuu ya KKKT ni pamoja na ***kuratibisha, kuwezesha na kufanya utetezi*** kwa manufaa ya Kanisa zima.

KKKT ina taasisi na vituo vinavyotunza Kazi za Umoja: **1.** Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira **2.** Seminari Ndogo ya Kilutheri Morogoro **3.** Kituo cha Redio Sauti ya Injili, Moshi. **4.** Shule za Msingi kwa watoto viziwi Mwanga na Njombe. **5.** Shule ya Sekondari kwa watoto viziwi Njombe. **6.** Miradi ya kuongeza kipato.

Pamoja na vituo vya Kazi za Umoja, Dayosisi zina hospitali 23 na zahanati / vituo vya afya 150. Dayosisi zote zina shule za msingi, sekondari na vyuo vya ufundi na maarifa mbalimbali. Baadhi ya Dayosisi zina vyuo vikuu. Taasisi hizi hutoa huduma kwa watu wote bila ubaguzi.



Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo.

Karibu kila dayosisi /taasisi zake/ idara zina miradi midogo midogo ya kuinua kipato; miradi ya maji salama, miradi ya ng'ombe wa maziwa, nk. Dayosisi nyingi zina miradi mikubwa na ya kati. Baadhi zimeanzisha mabenki au vyama vikubwa vya kuweka na kukopa (SACCOs).

## Kazi za Misioni

Kanisa limehisika na kusaidia uanzishwaji Kanisa la Kilutheri nchini Kenya, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Msumbiji, Malawi na Uganda. Pia linalea Kanisa la Kilutheri Zambia, Burundi na Rwanda. Ndani ya nchi maeneo ya Misioni ni Kigoma na Zanzibar.

## Ushirikiano na wengine

KKKT ni mwanachama hai wa: Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT); 'Lutheran Mission Cooperation' (LMC); Baraza la Makanisa Barani Afrika (AACC); Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF) na Baraza la Makanisa Duniani (WCC).

## Ofisi zilipo

Ofisi Kuu ya KKKT ipo Arusha "Lutheran Centre", Barabara ya Boma mkabala na Posta Kuu. Senta hiyo ina hosteli kwa ajili ya watumishi na wageni wa Kanisa.


**Kwa maelezo zaidi wasiliana na**

**Katibu Mkuu**

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania

**S.L.P.** 3033, **Arusha**

**Simu:** 250 8856/250 8857/**Fax** 254 8858

**Barua pepe:** elcthq@elct.or.tz

**Tovuti:** www.elct.org

Au **Tovuti:** www.elct.or.tz

**Uhuru na Amani**
Gazeti la KKKT
**Toleo la 2, 2018**
Na. 2 Vol. 118
**ISSN 0856 - 1214**

Uhuru na Amani ni Gazeti la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hutayarishwa na Kitengo cha Mawasiliano, KKKT.

Maoni yaliyomo katika makala zinazochapishwa ni ya mwandishi anayehusika na wala hayawakilishi mawazo ya Kanisa ama mhariri isipokuwa pale ambapo imetamkwa wazi. Ukiwa na maoni, ushauri, makala au maswali mwandikie:

**Mhariri**
**Uhuru na Amani**
**S.L.P. 3033**
**ARUSHA**
**Barua pepe:** elcthq@elct.or.tz
Simu: +255-27-250-8856/7
**Tovuti:** http://www.elct.org/

**MHARIRI**
**Elizabeth Lobulu**

Limepigwa Chapa na:
**Perfect Printers Ltd.**
S.L.P. 1487 Arusha +255 764 283 996
perfect@perfectprinters.co.tz

Newspaper Design & Typesetting:
**Elizabeth Lobulu**

**Wachangiaji wa Makala:**

Dkt. Agnes Abuom
Metropolitan Dkt. Mor Geevarghese Coorilos
Mch. Dkt. Olav Fykse Tveit
Mch. Jooseop Keum
Askofu Dhiloraj Ranjit Canagasabey
Askofu Conrad Nguvumali Sikombe
Nafkot M. Dessaleg

**PICHA YA JALADA:**

**Msalaba mmoja wapo uliotumika wakati wa Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti uliofanyika Hoteli ya Ngurdoto Arusha, mwezi Machi mwaka huu. Mkutano huo uliohudhuriwa na watu wapatao 1,200 uliitishwa na Baraza la Makanisa Duniani (WCC)** (PICHA NA WCC).

# MAONI YA MHARIRI

## Misioni ni wajibu wa kila mtu

**Watu wengi wanaosikiliza vituo vya Redio Sauti ya Injili, Redio Maria na Redio Habari Maalum walifahamu ujio wa wageni kutoka pande zote za dunia kwa ajili ya Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti (CWME) uliofanyika Hoteli ya Ngurdoto Machi 2018.**

**Neno kuu lilikuwa:** ***"Kuenenda kwa Roho: Wito wa Kuwa Wafuasi wa Mabadiliko".***

**Mkutano huo wa CWME yaani *Conference on World Mission and Evangelism,* uliohudhuriwa na washiriki wapatao 1,200; uliandaliwa na Baraza la Makanisa Duniani (WCC).**

**Washiriki walikuwa ni viongozi wa makanisa, wachungaji, wamisionari, wanafunzi wa theolojia, wadiakonia, watheolojia na watafiti kutoka makanisa, washirika wa ekumene na vyama vya misioni. Makanisa yaliyotuma washiriki si ya wanachama wa WCC pekee, bali hata ambayo si wanachama.**

**Katika maandalizi ya mkutano viashiria vya *kuenenda kwa Roho* vilionekana watu walipoweka tofauti zao pembeni hivyo umoja kiekumene ukawezekana. Kwa mfano, kamati ya maandalizi ya wenyeji, iliratibiwa na KKKT lakini wajumbe walitoka makanisa ya Jumuiya ya Kikristo Tanzania, Kanisa la Pentekoste, Kanisa Katoliki na Kanisa la Orthodox. Wajumbe hao walifanya kazi kama timu moja.**

**Hata ile siku ya kwanza ya mkutano Redio za makanisa hayo matatu zilifika na kurusha matangazo ya moja kwa moja ili kuwajuza wasikilizaji wao mambo yalivyokuwa. Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa ushirikiano kama huo kwa vyombo vya habari vya CCT, Katoliki na Pentekoste kuwa mahali pamoja ili kurusha habari za tukio moja kwa wakati mmoja.**

**Ratiba ya mkutano nayo ilikuwa shirikishi na hakuna mjumbe ambaye hakushiriki matukio yaliyo mengi hata pale ambapo mahubiri au mtoa mada anatoka katika madhehebu tofauti na yake.**

**Uchangamano, ushirikiano na umoja kiekumene ulijitokeza kiasi ambacho baadhi ya washiriki walisema Tanzania tunachakujifunza.**

**Soma makala mbalimbali katika gazeti hili uelewe zaidi kuhusu mkutano huo wa kihistoria.**

# Wito wa Ufuasi kutoka Arusha



Makanisa na jumuiya za kiekumene zijipime na kuondoa chembe za ubeberu katika mifumo na huduma.

## Tamko la Mkutano wa CWME

"Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti (CWME) uliandaliwa na Baraza la Makanisa Duniani (WCC) tarehe 8 -13 Machi 2018 Arusha, Tanzania. Watu zaidi ya 1,200 walishiriki. Washiriki wanahusika na kazi za Misioni na Uinjilisti kutoka madhehebu mbalimbali ya Kikristo na waliotoka pande zote za dunia.

Kwa bashasha kubwa tulisherehekea kwa msisimko na uhai utokanao na Roho wa Mungu aliye kati yetu hivi sasa. Washiriki walihamasika kwa kuwepo katika mazingira ya uamsho wa kiroho wa Kiafrika. Kwa njia ya Somo la Biblia, maombi, ibada na kushirikishana taarifa zetu kwa pamoja, tulitiana moyo wa kuendelea kushuhudia kuhusu Ufalme wa Mungu tulioupokea kwa maisha, kusulubiwa na kufufuka kwa Bwana wetu Yesu Kristo.

Licha ya kuwepo mwangaza hafifu wa matumaini, inapasa kutambua nguvu za mauti zinazotikisa ulimwengu na kusababisha mateso kwa wengi. Tumeshuhudia kwa mshangao mkubwa ulimbikizaji mali unaotokana na mfumo wa fedha wa kibepari unavyotajirisha watu wachahe na kuwafanya wengi wabaki fukara. Na hiki ndio chanzo kikuu cha vita, machafuko, uharibifu wa ekolojia, na mateso duniani.

Tunatambua wanaobeba mzigo mzito zaidi ni walio pembezoni. Mfumo huu wa kimataifa wenye nguvu kubwa umefanya soko la fedha kugeuka kuwa kama miungu kwa wakati wetu huu na kuimarisha utamaduni wa kukandamiza wengine kwa kubaguana, kuendelea kuwasukumia wengine kando na kuwatenga mamilioni ya watu hivyo kuwaacha katika mazingira yasiyo salama na ya kinyonyaji.

Masuala haya si mageni kwa mwaka 2018, bali Roho Mtakatifu anaendelea kutembea katika wakati wetu huu; akitutaka sisi jamii ya Wakristo tuitike haraka wito kuwa wafuasi wa mabadiliko katika ngazi ya mtu binafsi na kijamii.

Ufuasi ni zawadi na wito wa kushirikiana na Mungu ili kubadilisha ulimwengu. Katika kile ambacho wanatheolojia wa awali walikiita "imani ya utakatifu



Wito wa kuenenda kwa Roho ni kukubali kuubeba msalaba pamoja na Bwana Yesu.

(theosis)" au kuabudu vitu kama miungu (deification), tunashiriki neema kwa kushiriki utume wa Mungu. Safari kama hii ya ufuasi inatuongoza tushiriki na kuuishi upendo wa Mungu katika Yesu Kristo kwa haki na amani kwa njia ambazo ni tofauti na za kidunia (Yohana 14: 27). Kwa hiyo tunaitikia wito wa Yesu wa kumfuata tukianzia pembezoni mwa dunia.

Sisi wafuasi wa Yesu Kristo, iwe mtu mmoja mmoja na kwa pamoja, tulipobatizwa tulipokea wito wa kuwa wafuasi wa mabadiliko kwa kuwa na maisha yaliyounganishwa na Kristo katika dunia ambayo wengi wamekata tamaa, wamekataliwa, wapweke na wasiothaminiwa kabisa.

Tumeitwa kumwabudu Mungu mmoja wa Utatu, Mungu wa haki, upendo na neema wakati huu ambapo watu wengi wanaabudu miungu bandia kwa kujali tu mfumo wa soko.

Tumeitwa kutanganza *Habari Njema ya Yesu Kristo,* maisha tele, toba na msamaha wa dhambi na ahadi ya maisha ya milele. Tufanye haya kwa maneno na vitendo, kwa kuwa tuko katika dunia iliyo na vurugu ambapo watu wengi hutolewa kafara kwa ajili ya sanamu za miungu wa mauti. Na hadi sasa bado Injili haijawafikia watu wengi.

Kwa furaha tumeitwa kutenda apendavyo Roho Mtakatifu ambaye anawapa uwezo wa haraka watu walio pembezoni wa kutafuta haki na heshima yao. Tumeitwa kulitambua Neno la Mungu katika dunia inayowasilisha ujumbe unaopingana, wa uongo na wa kuwatatanisha watu.

Tumeitwa kujali uumbaji wa Mungu na kuwa na mshikamano na mataifa yaliyoathirika vibaya na mabadiliko ya *tabia nchi* kutokana na ukatili na ubinafsi wa kinyonyaji kwa kuwa binadamu kaamua kufaidika na mazao ya mazingira kwa uroho na kwa mfumo wa watu kuwa na matumizi yasiyo na mipaka.

Tumeitwa kama wafuasi tushirikiane pamoja ili katika jamii pawepo haki na kujaliana katika kutafuta umoja katika safari yetu ya kiekumene kwenye dunia inayowatenga watu na kuwaweka pembezoni kwa kuwabagua.

Tumeitwa kuwa wafuasi waaminifu wa Mungu anayetugeuza kwa upendo ili tushiriki mazungumzo na watu wa imani nyingine katika dunia ambapo siasa ndani ya mashirika ya kidini husababisha machafuko. Wito wetu ni kuwa viongozi ambao ni watumishi, wadhihirishe ufuasi wao kwa njia ya Kristo katika dunia ambayo inajali zaidi mamlaka, utajiri na utamaduni wa fedha.

Tumeitwa kuangusha kuta na kutafuta haki kwa ushirikiano na watu ambao wameporwa mali zao na kuwa wakimbizi nchini mwao; wakiwemo wahamiaji, wakimbizi na wanaotafuta makazi nje ya nchi zao na kupinga uwepo wa mipaka inayotenganisha na kusababisha kifo.

Tumeitwa kufuata njia ya msalaba, ambayo inatufanya tuone changamoto za utabaka kwa kutawala, upendeleo, uwezo wa kibinafsi na wa kimfumo.

Tumeitwa ili tuishi katika mwanga wa ufufuo, unaotoa matumaini – kujaa uwezekano wa mabadiliko. Huu ni wito wa ufuasi wa mabadiliko.

Huu siyo wito tunaoweza kuuitikia kwa nguvu zetu wenyewe, hivyo hatimaye wito huu ni wito wa kufanya maombi:

***Ee Mungu wa upendo, tunakushukuru kwa zawadi ya maisha katika mapana yake ya utofauti na uzuri wake. Bwana Yesu, uliyesulubiwa na kufufuka, tunakusifu kwa kuwa ulikuja kutafuta kondoo aliyepotea, kuwaweka huru wanaonyanyaswa, kuponya wagonjwa na kuwageuza wenye ubinafsi. Ee Roho Mtakatifu, tunafurahi kwa kupuliza punzi ya uhai duniani na kujimimina katika mioyo yetu. Kadiri tunavyoishi kwa Roho tunaomba pia tuenende kwa Roho. Tupe imani na ujasiri wa kujitwika msalaba wetu na kumfuata Yesu - kuwa mahujaji wa haki na amani katika zama zetu hizi. Kwa baraka ya watu wako, utunzaji wa dunia na kwa utukufu wa jina lako. Kwa njia ya Kristo Bwana wetu. Amen.***"

Tafsiri na Elizabeth Lobulu. Picha na Albin Hillert/ WCC.

KKKT

ELCT

# Mkutano wa Dunia wa Misioni

# TOLEO MAALUM

## BAADA YA MKUTANO - CWME

# Mkutano watoa tamko la pamoja



**Dkt. Agnes Abuom, Mwenyekiti wa Vikao vya Kamati Kuu WCC, aliyefungua Mkutano na kusoma Tamko la Mkutano siku ya kufunga. Soma tamko hilo katika ukurasa wa 4 wa toleo hili.**

"Afrika ni kituo muhimu cha hija katika safari ya kutafuta haki na amani duniani na ndio sababu Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti (CWME) umerudi tena Afrika baada ya miaka 60". Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Vikao vya Kamati Kuu Baraza la Makanisa Duniani (WCC), Dkt. Agnes Abuom, alipokuwa akifungua mkutano huo.

Alisema: "Mkutano uwe fursa ya kujadili na kuhoji waziwazi kama mbinu za misioni zitumikazo sasa zina lengo la kuleta uhai au ni chanzo cha mateso na mauti kwa watu?

"Wito wa misioni na ufuasi utuwezeshe kubadilisha maisha ya watu na jamii ikubali na kuheshimu *utukufu wa sura ya Mungu katika kila mwanadamu* na pasiwepo mtu yeyote atakayebaguliwa kwenye mchakato endelevu katika kuleta amani, haki na kuufaidi utajiri wa dunia," Dkt. Abuom alisema

Katibu Mkuu wa Baraza la Makanisa Duniani (WCC), Mchg. Dkt. Olav Fykse Tveit, aliwashukuru washiriki wote wa Mkutano huo aliouelezea kuwa ni wa kipekee na kihistoria.

Mkutano huo wa 14 umefanyika katika hali ya sherehe kwa kuwa mwaka 2018, WCC inatimiza miaka 70. Miaka 60 iliyopita mkutano wa aina hii ulifanyika Achimota, Ghana.

Alisema: "Tuna wito wa kuleta mabadiliko ya kweli kama anayoyataka Mungu kwa manufaa ya umma na kwa yeyote Mungu anayemjali.

"Kauli mbiu ya Mkutano inatupa wito wa *ufuasi wa mabadiliko kwa kuenenda kwa Roho,* hivyo tuguse hisia za wanao -tuzunguka kwa kuhakikishia amani na haki vinapatikana bila ubaguzi au kumwacha mtu yeyote nyuma. "Si



**Mch. Dkt. Olav Fykse Tveit, Katibu Mkuu wa Baraza la Makanisa Duniani.**

lazima kwenda masafa ya mbali ili uoneshe ufuasi wako.

"Kwa kufuata na kuwasaidia majirani zako walio wahitaji, huko ndiko kueneza Injili ya kweli. Na tuwajibike kuutunza uumbaji wote wa Mungu kwani tuna ulimwengu mmoja tu, hatuna mahali pengine pa kuishi," alisema.

Mkutano huo ulioandaliwa na WCC ulihudhuriwa na watu zaidi ya 1,200 wakiwemo viongozi wa makanisa, watafiti, wanafunzi wa theolojia, wachungaji, wamisionari, madiakonia, na watheolojia kutoka makanisa, washirika wa kazi za ekumene na vyama vya misioni. Kwa maelezo zaidi funga tovuti: www.oikoumene.org/en/resources/documents/commissions/mission-and-evangelism/



**Maandamano kabla ya kufunguliwa Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti. "Tunaitwa kuwa wafuasi wa mabadiliko kwa kuishi maisha yaliyounganishwa na Kristo katika dunia ambayo wengi wamekata tamaa, wamekataliwa, wapweke na wasiothaminiwa kabisa".** (Picha na WCC)

KAULI MBIU - *Kuenenda kwa Roho: Wito wa kuwa wafuasi wa mabadiliko*


World Council of Churches


# Isiwe kugeuza bali kupindua

**Na Elizabeth Lobulu**



Metropolitan Dkt. Mor Geevarghese Coorilos, Mwenyekiti Kamisheni ya Misioni na Uinjilisti ya Dunia WCC.





Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo, Mwenyeji wa CWME, alisema: "Wajumbe wa mkutano wakiongozwa na Roho Mtakatifu, wako katika hija ya kuleta mabadiliko duniani."



Mkurugenzi wa Kamisheni ya Misioni na Uinjilisti ya Dunia, WCC, Mch. Dkt. Jooseop Keum.



Mchg. Dkt. Elieshi Mungure, Mtanzania ambaye ni Katibu wa Afrika katika Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani, akielezea kuhusu msalaba wa mpingo waliopewa washiriki wote wa Mkutano wa 14 wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti (CWME).

Picha zote na WCC

"Kanisa kila siku liko safarini linapofanya kazi za misioni," Metropolitan Dkt. Mor Geevarghese Coorilos, kutoka India ambaye ni Mwenyekiti wa Kamisheni ya Dunia ya Misioni na Uinjilisti ya Baraza la Makanisa Duniani (WCC), aliyasema hayo wakati wa Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti (CWME).

Kauli mbiu ya mkutano huo ilikuwa: ***"Kuenenda kwa Roho: Wito wa kuwa wafuasi wa mabadiliko".***

"Katika dunia inayoongozwa na ubeberu, inabaidi yafanyike mageuzi na wala si kubadilisha tu. Katika dunia ambapo nguvu za mwanadamu na fedha zinakusudia kupokonya mamlaka ya Mungu njia pekee ya kubadilisha hili ni kwa kupindua dunia kichwa chini miguu juu," Metropolitan Dkt. Coorilos alisema.

Akisoma ripoti yake: "*Kutoka Athens hadi Arusha,"* Mch. Jooseop Keum, Mkurugenzi wa Kamisheni ya Dunia ya Misioni na Uinjilisti, alisema Afrika siyo tena eneo la kufanyiwa misioni kwa kuwa misioni inaanzia kokote kuelekea kila upande ndio maana uongozi wa kazi za misioni kwa mtazamo mpya, uko Afrika.

Aliwataka washiriki toka duniani kote watumie fursa ya kuhudhuria mkutano huo, kuendeleza mambo mazuri waliyojifunza kutoka Afrika.

Mchg. Keum anayetoka Korea, alisema mkutano ulijionea namna Afrika ilivyo na utajiri mkubwa wa madhehebu mbalimbali ya Kikristo, mshikamano, udugu na uamsho wa kiroho.

Mchg. Dkt. Susan Durber, Mwenyekiti wa *Kamisheni ya Imani na Ushirika (Faith and Order)* alisema: "Safari ya kuelekea umoja kiekumene inaanza na misioni. Ukiangalia Mkutano wa Kwanza wa CWME uliofanyika Edinburg, Uingereza 1910 au ukisoma andiko la karibuni la *Kamisheni ya Imani na Ushirika,* utaona hatua ya kwanza ya kufikia umoja lazima ianze na misioni.



Dkt. Susan Durber, Mwenyekiti Kamisheni ya Imani na Ushirika, akiongoza *"Warsha kuhusu Ufuasi katika Huduma ya Kichungaji*" wakati wa Mkutano wa 14 wa CWME.

"Siku zote tunapo -itika wito au kukubali utume, tujue misioni hiyo ni ya Mungu na lengo si kujijengea himaya zetu binafsi bali ni kwa ajili ya Kristo Yesu anayedhihirisha uwepo na kusudi la Mungu.

"Kila mmoja pamoja na tofauti alizonazo anamhitaji na kukamilishwa na mwenzake. Tofauti hazipo tu katika jamii bali hata katika makanisa. Na kwamba Mungu analeta umoja hata miongoni mwa waliotofauti na ndio maana Kristo anatualika ***"wote wawe na umoja".*** Kamisheni hiyo ndio inayounganisha makanisa hata yale ambayo siyo wanachama wa WCC. Dkt. Durber aliongoza warsha kuhusu *Ufuasi katika Huduma ya Kichungaji* wakati wa Mkutano huo.



Mchg. Dkt. Janet Corlett kutoka Kanisa la Methodist Uingereza, aliongoza kipindi cha kufunga mkutano. Alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maisha ya Kiroho katika Mkutano. Yeye ni Makamu Mwenyekiti wa vikao vya Kamisheni ya CWME.

# Alikaneni wakati wa matukio yenu - Askofu Nassari

Na Elizabeth Lobulu

**Yafuatayo ni maoni ya washiriki waliowakilisha Makanisa ya Tanzania katika Mkutano wa 14 wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti:**

Askofu Elias Kitoi Nassari kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Meru alisema: Ushirikiano uliooneshwa katika mkutano uliomalizika wa Dunia wa Misioni na Uinjlisti hautofautiani na ushirikiano uliopo wa makanisa chini ya Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT).

Askofu Nassari alisema ni fursa yake ya kwanza kuhudhuria mkutano huo wa kiekumene wa kimataifa. Mkutano kama huo uliofanyika Afrika mara ya kwanza miaka 60 iliyopita jijini Achimota Ghana. Askofu Nassari anayetoka KKKT Dayosisi ya Meru alisema lengo la mkutano ni kutafuta namna bora zaidi ya kufanya utume tuliopewa na Yesu Kristo wa kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi.

Alishukuru Baraza la Makanisa Duniani (WCC) lililoandaa mkutano huo na kuishukuru Tanzania kwa kuwa na hoteli ya Ngurdoto iliyopokea mkutano. Kuhusu jambo alilojifunza katika mkutano huo alisema sasa makanisa ya Tanzania yamefunguliwa macho, hivyo viongozi wasiwe waoga kualikana katika matukio. Alisifu mkutano kwa kuwa na harufu ya Kiafrika na ingeshangaza kama ingekuwa kinyume chake.

Alipendekeza kwamba katika mikutano kama hiyo ingefaa mwaliko ungeenda kwa maaskofu wengi zaidi wa Kiafrika ili wasaidie kuendeleza kazi za kiekumene kwani wakati mwingine wanakuwa kikwazo.



Askofu Eliaski Kitoi Nassari wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) alimwakilisha Mkuu wa KKKT kufungua Kongamano la GETI. Kulia ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Mch. Prof. Joseph Parsalaw, aliyekuwa mwenyeji wa Kongamano na kushoto ni Dkt. Rogate Mshana, Mwenyekiti wa Kamati Wenyeji ya Maandalizi ya Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti (CWME).

# Tujenge amani na umoja

Katibu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Bw. Brighton Killewa, ameshukuru makanisa chini ya Jumuiya ya Makanisa Tanzania (CCT), Kanisa Katoliki na Kanisa la Orthodox kwa kuonesha ushirikiano mkubwa wakati wa maandalizi ya Mkutano wa 14 wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti.

"Ule umoja tunaotakiwa tuwe nao kwa kiasi chake umejidhihirisha katika mkutano huu kwamba sote tunaunganishwa na Yesu Kristo. Hivyo tunahitajiwa kujenga hali ya amani na umoja wakati wote," alisema.



Bw. Brighton Killewa, Katibu Mkuu wa KKKT.


# Tofauti ni dalili za utajiri na ukamilifu

Askofu Conrad Nguvumali Sikombe, wa Kanisa la Moravian Jimbo la Rukwa alisema: "Neno kuu la Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti unataka washiriki na watu wote kutembea katika Roho Mtakatifu tukipeleka Injili kama wanafunzi wa Yesu licha ya tofauti zetu. Hivyo tunapaswa kukazana kubadilisha ulimwengu kwa njia ya Roho Mtakatifu ili watu wamjue Yesu Kristo na kuwapelekea *Habari Njema* badala ya dunia iliyojaa habari mbaya.

"Katika karne ya 21 tunaitwa kutangaza habari nzuri kama vile mwanamke kisimani alivyoalika watu waje wasikie habari kwa Yesu. Na sisi tukitoka katika mkutano huu, habari tunazopaswa kwenda kutangaza katika umoja wetu: Walutheri, Wamoravian, Wabaptisti, Waanglikana, nk., ni kuwaelekeza watu kwa Yesu Kristo.

"Watu wasiendelee kusikia tu habari mbaya zenye kuwapa maumivu. Na tusibaki tu katika kueneza Injili bali hata habari nzuri zinazohusu mabadiliko kwa kuwapa huduma za afya wagonjwa wapone; shule ili kuondoa ujinga na jamii ipone kiakili, kimwili na kiroho.

"Tumekumbushana katika mkutano kwamba tusiangalie tu habari za kwenda mbinguni ila watu wafurahie maisha kwa kuonja uumbaji wa Mungu watu wakiwa hapa duniani na baadaye wakaishi katika furaha ya uzima wa milele.



Askofu Conrad Nguvumali Sikombe, Kanisa la Moravian Jimbo la Rukwa.

"Tofauti zetu kuhusu masuala ya ubatizo, namna ya kuabudu na hata mavazi, yote hayo yanatuonesha utajiri na ukamilifu wetu kama Kanisa.

Ingechosha kama katika mkutano mzima tungekuwa na namna moja tu ya kufanya mambo yetu. Tofauti hizi zinaonesha ni namna gani Yesu Kristo anavyoheshimiwa, anavyosifiwa na anavyoabudiwa," Askofu Sikombe alifafanua.

# Wanawake wanamchango muhimu kazi za misioni



**Mkutano wa maandalizi kwa wanawake ulifunguliwa na Metropolitan Dkt. Mor Geevarghese Coorilos, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Dunia ya Misioni na Uinjilisti katika Baraza la Makanisa Duniani. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni hiyo, Mchg. Dkt. Janet Corlett wa Kanisa la Methodist, Uingereza.**

Wanawake waliohudhuria Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti walikuwa na mkutano wao wa maandalizi katika Hoteli ya New Safari, Arusha, tarehe 6 hadi 7 Machi, 2018.

Wajumbe walipokea taarifa iliyoonesha kwamba wanawake wako mstari wa mbele katika kazi ya misioni ya Mungu (missio dei) yaani kutangaza Injili na walitaka taarifa kama hizo ziwekwe kwenye kumbukumbu za kihistoria.

Walisema kama walivyo wanaume, wanawake wana maono na wanajitoa kwa hali na mali katika huduma mbalimbali za kuanzisha na kuendeleza misioni ndani na nje ya nchi zao. Pia wanashiriki harakati za kutafuta haki, uwezo kiuchumi, katika jamii na kuhusika kutoa huduma za afya.

Wameeleza kwamba hakuna mazingira rafiki ya kuwezesha wanawake wengi kujifunza na kufanya kazi za theolojia. Wanawake wanapewa mshahara mdogo kuliko wanaume wenye sifa na taaluma ileile. Imeonekana kwa muda mrefu uzoefu na mawazo ya wanawake hayazingatiwi katika mitaala. Wanawake wanakumbana na ubaguzi kutokana na tofauti za mila, desturi na utamaduni zinazokinzana na ***Habari Njema.***

Upo ubaguzi kwa watu wenye ulemavu. Mifumo na miundo kandamizi imesababisha ubaguzi na kuwepo biashara ya kusafirisha na kuuza watu utumwani.

Historia imeonesha jinsi wakristo wanavyoishi kinyume na maagizo ya Injili kwa kushiriki katika mifumo ya unyonyaji kiuchumi kwa kujitwalia raslimali katika mataifa ya kusini mwa dunia na kusababisha njaa, umaskini, migogoro na vita visivyoisha.

Japo kuna baadhi ya makanisa yaliyokiri na kutubu kwa kuhusika katika uonevu na unyonyaji huo, wanawake wameona hilo halitoshi. Baada ya kutubu makanisa hayo yanapaswa kuchukua hatua kwa kushiriki kurekebisha uovu huo na madhara yake.



Wanawake hao wanatoa wito kwamba washiriki wa mkutano waungane nao kuyaambia makanisa, vyama vya misioni na washirika wa kiekumene waandae nyenzo za mafunzo ili kusaidia watu waondokane na mafundisho potofu yaliyofanya pawepo mifumo kandamizi isiyojali maisha ya binadamu. Walitaka pawepo uhamasishaji kwa Serikali ili zitekeleze malengo ya milenia ufikapo mwaka 2030.

**TAFSIRI NA: ELIZABETH LOBULU.**
**PICHA ZOTE NA WCC.**









# Tushirikiane kueneza Injili - Gulle



**Askofu Andrew Gulle,**
**KKKT Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria.**

Askofu Andrew Gulle wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki ya Ziwa Victoria, alisema: "Umoja na mahusiano katika Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti umeamsha ari ya kujitambua kwamba wakristo wote bila kujali tofauti zetu za mapokeo, madhehebu, makabila, rangi au lugha, ***tumeitwa kuwa wanafunzi wa Yesu ili kutangaza Injili.***

Tofauti zisitufanye kuacha wajibu wetu wa msingi wa kuhubiria watu ili kuleta mabadiliko kwa kumtangaza Kristo.

"Kwamba mbinu zinazotumika kuwafikishia watu ***Habari Njema*** ni za Walutheri, Waorthodox, au Wamoravian; si muhimu kwa kuwa tunapaswa kuwahubiri watu Injili na kuleta mabadiliko katika dunia: kimwili na kiroho.

"Ujumbe kutoka Mkutano wa Misioni ni kwamba umoja unasisitizwa zaidi na kila mmoja atimize wajibu wake," Askofu Gulle alisema.

# Injili isonge mbele: Vijana wanataka mageuzi

Ukristo na mahudhurio kanisani kwenye nchi za magharibi unapungua lakini katika nchi zinazohesabika ni za pembezoni ukristo unakua kwa kasi; hamasa ya kuendeleza kazi ya Injili na hali ya kiroho inakua na mijadala ya kitheolojia inapamba moto.

Hayo yalisemwa na Adi Mariana Waqa kijana kutoka Kisiwa cha Fiji, alipokuwa anatoa mada katika Mkutano wa 14 wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti.

Alisema ukweli ni wazi kwamba watu walio pembezoni mwa jamii; ambao utamaduni au nchi zao ziliwaweka kando, kwa sasa ndio wanaoendeleza misioni kwa nguvu zaidi. Alitaka wakristo *wafanye mageuzi* katika kazi za misioni na wala si mabadiliko tu.



Bi Adi Mariana Waqa (katikati) akishiriki matukio katika mkutano wa 14 wa CWME. (Picha zote na Albin Hillet/ WCC)



Mchg. Dkt. Mutale Mulenga-Kaunda toka Chuo Kikuu cha KwaZulu-Natal, Afrika Kusini akitoa mada siku ya ufunguzi kuhusu hatma na ukombozi wa vijana wa kike wa Kiafrika.

# Ufuasi unakuwepo kwa kujitolea kwetu

"Ufuasi unakuwepo kwa kuchukua hatua, kujitolea na kuishi kila dakika ukiwa umekubali kumfuata Yesu."

Hayo yalisemwa na Askofu Dhiloraj Ranjit Canagasabey, alipotoa mada wakati wa Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti (CWME) mnamo Machi 12.

Askofu Canagasabey ambaye ni Mkuu wa Kanisa la Anglikana la Ceylon, Colombo alisema: "Huwi tu mfuasi kwa kubatizwa peke yake bali ni kwa kuishi kwa matendo mafundisho yaliyoamriwa na Yesu.

Bi Nafkot M. Dessaleg, mtheolojia kijana toka Ethiopia alisema kwa kuwa Yesu aliweza kuwafundisha wanafunzi 12 katika kipindi cha miaka mitatu, hivyo akatoa changamoto kwa washiriki nao wakafundishe watu 12 katika miaka mitatu wawe wanafunzi wa Yesu ili waweze kukataa maonevu ya kidunia na kulipenda neno la Mungu katika maisha yao ya kila siku.




Imani inayobadilisha ni chanzo cha matumaini, haki, amani, upendo na kusimamia ukweli bila ubaguzi.

Mchg. Dkt. Mutale Mulenga-Kaunda, kutoka Chuo Kikuu cha KwaZulu- Natal, Afrika Kusini akitoa mada ya kwanza katika mkutano alisema: Waafrika katika kutafuta majibu ya maswali yanayohusu maisha na kifo wanaishi kiekumene kwa kuwa wamezungukwa na utamaduni wao wa asili, uislamu, na mitazamo mbalimbali ya kikristo duniani.

Alisema matunda na raslimali za kazi ya misioni barani Afrika hutumika kwa manufaa ya watu wote katika jamii ili kudumisha uhai.

Dkt. Mulenga-Kaunda alitoa mfano wa malezi yake jinsi alivyolelewa kiekumene katika maisha yake ya kiroho jambo lililowagusa wajumbe na kusababisha majadiliano motomoto.

Akijadili mada ya Kaunda, Mchg. Dkt. Upolu Lumā Vaai, Mkurugenzi wa Theologia Chuo Kikuu cha Theolojia cha Pacific-Fiji, alisema: "Inatupasa tukubali kuishi katika familia huku tukithamini uhusiano wetu na mazingira. Licha ya tofauti za rangi, jinsi na utambulisho tunauhusiano katika asili ya uumbaji wetu," alisema Vaai.

Profesa Mstaafu Néstor O. Míguez, Mtheolojia wa Argentina, alisema maisha tunayopitia au tuliyopitia yametuandaa na kutupa nguvu kwa ajili ya kufanya kazi za misioni.

# Mkutano umetoa picha halisi ya umoja

**"Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti ulioandaliwa na Baraza la Makanisa Duniani (WCC) umetoa picha halisi ya umoja wa Kanisa la Mungu linavyofahamika duniani." Hayo yamesemwa na Askofu Ambele Mwaipopo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) aliyekuwa mmoja wa wajumbe wa KKKT katika mkutano huo ulioandaliwa kwa ajili ya washirika wa misioni na uinjilisti. Katika ukurasa huu kuna maoni ya watu mbalimbali.**



Askofu Ambele Mwaipopo,
KKKT Dayosisi ya Ziwa Tanganyika.

Mchg. Dkt. Faustin Mahali, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (Utawala) alisema:

"Mkutano umeonesha kwamba moyo wa ushirikiano miongoni mwa makanisa upo. *Tofauti za udhehebu zisiwe msingi wa mahusiano ila mkazo uwe kwamba sote tu wakristo na kwamba sisi ni binadamu tulioumbwa kwa sura na Mfano wa Mungu.*



Mchg. Dkt. Faustin Mahali,
Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (Utawala).

"Katika ngazi ya kimataifa ziko juhudi za mikutano ya wataalamu na wana- theolojia na majarida mengi yametolewa. Roho hiyo inabidi ilelewe na kuimarishwa kwa kushirikisha kada za chini. Makanisa chini ya Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) yashirikiane zaidi ya kuwa na miradi ya pamoja ya huduma za kijamii au vikao vya viongozi wa juu peke yake.

"Wakati umefika wa kuimarisha umoja kwa kuamsha ari na mazungumzo hata katika ngazi za sharika, jimbo, mtaa, nk.," Alisema Dkt. Mahali.

Askofu Mwaipopo alisema: "Upekee wa mkutano huu umetokana na ushiriki wa watu kutoka pande zote za dunia wakiwakilisha makanisa ya Kilutheri, Morovian, Anglikana, Baptisti, Orthodox na Katoliki. Japo Kanisa Katoliki si mwanachama wa WCC lakini ni mjumbe katika *Kamisheni ya WCC ya Imani na Ushirika (Faith and Order)*. Pia ni mshirika wa WCC katika kutoa huduma za kijamii kiekumene. "Mkutano ulipokea salamu kutoka kwa Papa Francis uliosomwa na Askofu Brian Farrel, mwakilishi wa Vatican. Pia Balozi wa Vatican nchini na Mhashamu Kadinali Polycap Pengo walihudhuria.



**Dkt. Rogate Mshana (kushoto), Mwenyekiti wa Kamati Mwenyeji iliyoandaa Mkutano wa 14 wa CWME 2018 akiwa na Mkurugenzi wa CWME Mch. Jooseop Keum.**

Dkt. Rogate Mshana, Mwenyekiti wa Kamati Mwenyeji iliyohusika kuanda mkutano aliongea kuhusu Tamko linalopatikana ukurasa wa 4 akisema:

"Kwanza kabisa **Tamko** linataka tuendelee kumwabudu Mungu mmoja wa upendo, ufuasi na mletaji wa neema. Hayo yafanyike katika wakati duniani pia kuna miungu ya uongo. Watu katika mifumo ya kibiashara humwaga damu za watu kwa kutoa kafara kwa 'miungu ya mauti'.

Jambo la pili, Tamko linaonesha Roho Mtakatifu anawavuvia hata watu wa pembezoni walioumizwa, kudharauliwa na wasiojua jinsi ya kupata haki zao.

Na jambo la tatu tunahimizwa kufundisha ***Habari Njema*** za Yesu Kristo kwa kuishi maisha yenye uzima tele, yaliyojaa neno na matendo katika ulimwengu wenye ukatili ambapo watu wengi wanatolewa kafara kwa uchu wa mali au umaarufu duniani. Pia Baraza la Makanisa Duniani (WCC) linajitahidi kuhamasisha makanisa na mashirika ya kimisioni yasambaze ujumbe kwamba na sisi wenyewe inatupasa kujibadilisha.

Japo Kanisa la Orthodox limegawanyika lipo Kanisa la Magharibi na Kanisa la Mashariki, wajumbe wa mkutano walitiwa moyo kuwaona wawakilishi wao. Kwa mshangao mkubwa walipokea salamu za Papa Bartholomew I wa Kanisa la Magharibi la Orthodox zilizowasilishwa kwa njia ya video. Haya yanadhihirisha makundi yote yanaona umuhimu wa umoja wa Kanisa.

"Mada ziliongozwa na maprofesa wa makanisa yote na ushirikiano mzuri ulikuwepo watu walipoeleza wanachokiamini kwa uhuru. Na mkutano ukatoa tamko (angalia ukurasa wa 4). Washiriki walijifunza kutoka kwa washiriki wenzao kwamba, siyo kila mbinu na mpango ya misioni unafaa katika mazingira yote au kwa wakati wote. Hili lilizingatiwa na watoa mada na hasa wakati wa majadiliano ya makundi kila mtu alikuwa huru kujieleza," Askofu Mwaipopo alisema.



**Mchg. Lazaro Rohho (kushoto), Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti KKKT, akiongozana na Balozi wa Vatikan nchini, Askofu Mkuu Marek Solczyński, alipowasili mkutanoni.**

Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti KKKT, Mchg. Lazaro Rohho, alisema anamshukuru Mungu kwa kuwa Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti ulivyofanyika Arusha kama ilivyopangwa.

Alisema alikutana na watu toka maeneo, makanisa na medhehebu mbalimbali duniani waliokubali kukaa pamoja kwa umoja kwa kuwa anayetuunganisha ni Yesu Kristo.

Amejifunza kwamba ili kazi ya Injili isonge mbele kuna umuhimu kwa kila mhusika kujitoa kwa kutimiza kwa ukamilifu wajibu wake. Alifurahishwa kwa jinsi baadhi ya watoa mada waliofundisha na kutoa uzoefu wa safari ya kazi ya misioni duniani na watafiti waliojitoa kufanya tafsiri sahihi ya Biblia kutoka lugha ya Kigiriki kwenda lugha zao za kiasili (Kiafrika).

Alipongeza Baraza la Makanisa Duniani (WCC) kwa mipango mizuri iliyoonesha utaratibu mzuri uliokuwa umepangwa hata kwaya na maigizo ya watoto yaliendana na wazo au maudhui ya neno kuu.


# Salamu zatolewa





Mkutano wa 14 wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti ulikuwa mkubwa na kuwajumuisha watu wengi zaidi kuliko huko nyuma. Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa Kamisheni ya Dunia ya Misioni na Uinjilisti WCC, Mch. Jooseop Keum, alipokutana na waandishi wa habari siku ya ufunguzi wa mkutano.

Kiongozi wa Kanisa la Orthodox la Magharibi, Papa Bartholomew I alitoa ujumbe wa kutakia heri mkutano kwa njia ya video akiwatia moyo wote waliohudhuria kwa pamoja walete haki na amani katika jamii na baina ya makundi ya kiimani duniani.



**Askofu Brian Farrell, Katibu wa Baraza la Kipapa linalohamasisha Umoja wa Kikristo duniani (PCPCU).**

Mkuu wa Kanisa Katoliki, Papa Francis, alituma salamu zilisomwa na Askofu Brian Farrell wa Kanisa la Ireland ambaye ni Katibu wa Baraza la Kipapa linalohamasisha uwepo wa Umoja wa Kikristo Duniani (PCPCU).

Ujumbe wa Papa unasema: "Mmetoka pande zote za dunia kuhudhuria mkutano katika roho ya mkutano wa kwanza wa Dunia wa Misioni uliofungua ukurasa mpya baina za jumuiya za kikristo katika wito wa misioni. Nawakumbusha kuwa kazi ya Roho Mtakatifu inaanza wakati wa Ubatizo ambao ni wakati wa mabadiliko unaowaunganisha wakristo wote kwa Kristo katika umoja ambao tunahitaji kuuonesha wazi wazi ili dunia ipate kusadiki (Yn. 17: 21)," alisema.

Katika salamu zake Askofu Mkuu Justin Welby wa Kanisa Kuu la Anglikana la Canterbury, Uingereza alisema tuungane na mitume wa kwanza ambao kwa kukubali utume wao walisema "ufalme wako uje duniani."



**Mkuu wa Kanisa la Orthodox la Magharibi, Papa Bartholomew I.**

Mkuu wa Kanisa la Orthodox la Mashariki na Syria, Papa Nor Ignatus Aphrem II, alisema: "Tumfuate Yesu, tuache kujipenda nafsi na kusahau uhitaji wa majirani na wanaotuzunguka."

Alitoa mifano jinsi watu wa Syria wanaoishi maeneo yaliyotekwa na magaidi wanavyoteseka. Alisema ili kuwapa matumaini watu hao anaalika jumuiya ya kimataifa kuunga mkono juhudi za makanisa ya Syria kusaidia walioathirika na vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini humo.



**Mkuu wa Kanisa la Orthodox la Mashariki na Mkuu wa Kanisa la Syria, Papa Nor Ignatus Aphrem II.**

Katibu Mkuu wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), Mchg. Dkt. Martin Junge, alitoa salamu zilizosomwa na Mkurugenzi wa Misioni na Maendeleo FMKD kwa wakati huo, Mchg. Dkt. Fidon Mwombeki.



**Profesa Dkt. Dimitra Koukoura, Kanisa la Magharibi la Orthodox.**

Prof. Dkt. Dimitra Koukoura wa Kanisa la Magharibi la Orthodox alisema upo umuhimu wa kuwasha upya moto wa ushuhuda wa Kikristo katika nchi za ulaya. Alisema moto wa Injili kwa wakristo katika nchi za magharibi sasa umefifia.

Kule kukumbatia sana udunia, utandawazi, ubinafsi na kutojihusisha na dini ni baadhi ya sababu kuu za kudidimia kwa imani ya Kikristo ulaya.

Sababu nyingine ni kuibuka kwa utawala wa kidikteta uliodumu katika nchi nyingi karne ya 20 ambao ulitumia mbinu za kikatili kung'oa imani kwa Mungu wa upendo toka katika maisha ya kila siku; katika kumbukumbu na kutoka mioyoni mwa wakristo. Japo mwishoni mwa karne ya 20 serikali nyingi za kidikteta ziliangushwa lakini ikawa vigumu kupona kutokana na kirusi cha kutomjua Mungu kilichoingizwa kupitia mfumo wa kiuongozi.

Na Kipindi cha kuelimika (enlightenment age) kilileta mageuzi makubwa katika elimu na maarifa hasa katika nyanja za teknolojia ndio sababu watu wakaona wako juu ya imani ya dini. Kwa maelezo zaidi funga tovuti: www.oikoumene.org/en/resources/documents/commissions/mission-and-evangelism/

# Roho Mtakatifu atuongoze tulete mabadiliko duniani



**Mch. Dkt. Elieshi Mungure, Katibu Dawati la Afrika la Fungamano la Makanisa Duniani; Mch. Dkt. Olav Fykse Tveit, Katibu Mkuu wa Baraza la Makanisa Duniani (WCC); Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) wakiwa katika Ibada katika Usharika wa Nkuarungo, Mkoa wa Kilimanjaro 11 Machi 2018 pamoja na baadhi ya wajumbe wa Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti. Wengine pichani ni viongozi wa Usharika. Siku hiyo wajumbe hao wapatao 1,200 walishiriki ibada mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.** Picha na Albin Hillert/ WCC

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dkt. Fredrick Shoo, amewataka wajumbe wa Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti (CWME) waendelee kuongozwa na Roho katika hija ya mabadiliko ili duniani pawe mahali pa haki na amani na kuhuisha ahadi ya ufuasi kwa Kristo.

Hayo yalisemwa na Mkuu usiku wa 13 Machi 2018 wakati akiwaaga wajumbe zaidi ya 1,200 waliohudhuria mkutano wa 14 wa CWME.

Alisema Tanzania ni chimbuko la binadamu na nchi yenye milima Kilimanjaro, Meru, hifadhi za wanyama, ekolojia, maziwa na mito ambavyo kwa pamoja ni sehemu ya uzuri wa uumbaji wa Mungu ambao tunajukumu la kuulinda. "Kule kuona watu toka duniani kote wamefika mahali hapa tumeona ni ishara nzuri kwetu," alisema.

Makanisa yakiwemo ya Kiothodoki, Kilutheri, Anglikana, Katoliki na Pentekoste yaliwakilishwa na viongozi wa ngazi ya juu katika mkutano huo uliokuwa na Kauli mbiu: ***"Tukiishi kwa Roho na tuenende kwa Roho: Wito wa kuwa wafuasi wa mabadiliko."***



***ni*** **Katibu Mkuu wa WCC, Mch. Dkt. Olav Fykse Tveit, akihubiri katika ibada tare 11 Machi 2018.**



**Askofu Mary Ann Swenson wa Kanisa la United Methodist, Marekani (kushoto) akiwa na Dkt. Agnes Abuom (katikati), Mwenyekiti wa Vikao vya Kamati Kuu, WCC, akisoma tamko la washiriki wanawake katika Mkutano wa Dunia wa Misioni mnamo 8 Machi, Siku ya Wanawake Duniani. Kauli mbiu 2018: "Kutokomeza ubakaji na ukatili kwa wanawake."** (Picha na WCC)

## Ujumbe wa KKKT katika Mkutano wa 14 wa CWME



**Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo (watatu kulia), aliongoza ujumbe wa Kanisa katika Mkutano wa 14 wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti.** Picha na Elizabeth Lobulu

# 'GETI' inafundisha vijana masuala ya umoja kiekumene

Na Elizabeth Lobulu

Vikundi mbalimbali vilikutana kabla ya Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti na kimoja kilikuwa cha vijana 120 wakiwemo wanafunzi wa theolojia na elimu ya dini; watafiti wa umoja kiekumene; na wachungaji chini ya mwavuli wa 'GETI'. Huo ni ufupisho wa maneno *'Global Ecumenical Theology Insitute'.* Lengo la GETI ni kuhimiza na kuandaa vijana watakaokuwa watumishi au viongozi wa kazi ya misioni siku zijazo. Vijana hao watheolojia waliotoka vyuo na taasisi mbalimbali duniani; walikutana Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Arusha 5 - 7 Machi 2018 na baadaye wakajiunga na wajumbe wa Mkutano wa 14 wa CWME.



**Kama ishara ya kuendeleza uhai na huduma duniani, washiriki wa GETI walipanda miti Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.** (Picha zote na WCC)

Pamoja na mambo mengine, vijana hao walipokea na kujadili mada kuhusu: *Umoja Kiekumene; Mijadala ya Kitheolojia; Theolojia ya Kiafrika; Ukristo na Mwingiliano wa Theolojia na Utamaduni.*

Pia walishiriki warsha kwa Vijana iliyohusu *Misioni katika Vyuo na Shule za Sekondari na Huduma ya Vijana katika Makanisa na maeneo wanakotoka.*

Washiriki waliona upo umuhimu wa kubadili mbinu za kuwafikishia vijana Injili kwa sababu wanaona hali ya sasa imebadilika ikilinganishwa na zamani. Wanataka mikakati ya makusudi ifanyike kuwashirikisha zaidi vijana katika huduma.

Kwa kuona changamoto zao zinafanana, Vijana wa GETI katika warsha yao walitoa wito umoja wa kiekumene katika makanisa yote uimarishwe.

Walitaka mbinu za kufanya kazi ya kueneza Neno la Mungu zibadilishwe na ziendane na mazingira. Walihimiza kuwaendea na kuwafikishia watu walio pembezoni Injili ya upendo, haki na neema.

Pendekezo jingine kwa mkutano lilikuwa kuwaalika wakristo waishi maisha ya utume na ufuasi kwa kuhubiri Injili ya kweli ya Yesu Kristo.




**GETI ilitoa fursa kwa vijana kujifunza mijadala kuhusu masuala ya misioni na umoja kiekumene duniani.**



**Vijana walibadilishana mawazo na wakufunzi wao kuhusu njia mbalimbali za kuwashirikisha vizuri na kwa ufanisi zaidi vijana ili watoe huduma makanisani kwao hasa katika kufanya kazi za misioni.**



**Mkutano wa Dunia wa Misioni na Uinjilisti ulikuwa na timu ya waandishi wa habari toka nchi mbalimbali.**

# Wilson Sanga awa Askofu Kusini Kati

Askofu Wilson Benjamin Sanga, ameisifu Serikali chini ya Rais John Pombe Magufuli kwa jitihada inayofanya kukabiliana na rushwa na ubadhirifu wa mali za umma nchini.

Askofu Sanga aliyasema hayo wakati wa itikio lake baada ya kuwekwa wakfu na kuingizwa kazini kuwa Askofu mpya wa Dayosisi ya Kusini Kati kuchukua nafasi ya Askofu Lewis Sanga aliyemaliza muda wake.

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dkt. Fredrick Shoo, aliongoza Ibada hiyo ya wakfu.

Baada ya kuwekwa wakfu Askofu Sanga alimwingiza kazini Mch. Adili Sanga Pagallo kuwa Msaidizi wa Askofu Dayosisi ya Kusini Kati.

Katika itikio hilo, pia aliomba ushirikiano toka upande wa Serikali kwenye mradi wa Dayosisi wa kupata nishati ya umeme kwa kutumia nguvu ya maji ambao ulikuwa haujapatiwa kibali.

Alimwomba Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka asaidie kufikisha ombi hilo Serikalini kwamba kupitia Mamlaka ya Nishati Vijiji (REA) Dayosisi ya Kusini Kati iweze kupatiwa kibali ili mradi huo uweze kukamilika kwa wakati uliopangwa.

Mkuu huyo wa Mkoa aliiwakilisha Serikali katika ibada hiyo.

Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, alimpongeza Askofu Sanga na kumtaka awe mnyenyekevu, mwenye upendo, asiwe mnafiki wala kutegemea nguvu zake mwenyewe bali ategemee kuongozwa na Mungu na kutenda haki anapowahudumia watu. Pia alimshauri awe na ushirikiano na wale anaowaongoza ili jamii iwe na amani.

Mkuu wa Kanisa alikemea tabia ya baadhi ya viongozi wasio na ushirikiano wanaotumia vitisho ili kupitisha mambo wanayoyataka wao.

Katika hili alisema, baadhi ya viongozi hutaka kutumia nguvu za kishirikina ili kufanikisha matakwa kama hayo. Na akaomba Askofu Sanga asifike huko.



Askofu Wilson Benjamin Sanga, Dayosisi ya Kusini Kati.



Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mhe. Christopher Ole Sendeka akimpa zawadi Askofu Wilson Benjamin Sanga.



Baadhi ya viongozi waliohudhuria Ibada ya kuwekwa wakfu Askofu Wilson Benjamin Sanga wa Dayosisi ya Kusini Kati, Makete mjini tarehe 24 Juni 2018.

# Milango iko wazi kushauri Serikali



Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo, aliongoza Ibada ya kumweka wakfu, Mchg. Dkt. Isaac Kissiri Laiser, kuwa Askofu wa kwanza wa Dayosisi ya Magharibi Kati tarehe 10 Juni 2018. Dayosisi hiyo ni ya 26 ya KKKT. Kutoka kulia ni Msaidizi wa Askofu wa Dayosisi hiyo, Mch. Newton John Maganga, akifuatiwa na Askofu Laiser; Katikati ni Makamu wa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan; Mkuu wa KKKT na kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mheshimiwa Aggrey Mwanri.



Askofu Dkt. Isaac Kissiri Laiser, baada ya kuwekwa wakfu kuwa Mkuu wa Dayosisi ya Magharibi Kati.

Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, amesema milango ya Serikali iko wazi kwa viongozi wa dini kutoa ushauri na kukosoa.

Makamu wa Rais aliyasema hayo alipohutubia katika ibada na sherehe ya kumweka wakfu Askofu Isaac Kissiri Laizer kuwa Askofu wa kwanza wa Dayosisi mpya ya Magharibi Kati. Hapo awali ilijulikana kama Eneo la Misioni la Tabora. Uzinduzi huo unafanya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT liwe na dayosisi 26.

Mkuu wa KKKT alipongeza Serikali kwa jitihada za kupambana na rushwa na ufisadi na kukemea tabia iliyozuka ya watu wasio na nia njema kujaribu kupotosha mantiki ya tamko la kanisa lililotolewa wakati wa Kwarezma.

Waraka huo kwa washarika wa KKKT ulitolewa na Maaskofu wa KKKT na kupata idhini ya Halmashauri Kuu ya KKKT, pamoja na mambo mengine ulihusu hali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa nchini kwa lengo la kuangaliza mapungufu ili hatua stahiki zichukuliwe.

Askofu Shoo alimtaka Askofu Laizer aepuke kutawaliwa na kiburi cha madaraka. Alimshauri asikubali kurubuniwa na mtu yeyote bali atunze usafi wa kanisa kwa kutumika kwa uaminifu.

Pia alimtaka atunze roho za watu, kumhudumia mtu kiroho na kimwili, kutoa na kutetea haki na heshima ya mwanadamu hasa walio wanyone na wanaoteseka.

Askofu Laizer alisema atatoa ushirikiano na kuunga mkono Serikali



Askofu Dkt. Solomon Massangwa kushoto, Askofu Charles Mjema na Askofu Dkt. Alex Mkumbo wakishiriki tendo la kumweka wakfu Askofu Dkt. Kissiri Laizer.

# Viongozi wa Makanisa ya Kilutheri Tanzania na Marekani wakutana




Picha za viongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani na wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania waliokutana Moshi 6 - 9 Agosti, 2018.



Askofu Brian Maas kutoka Sinodi ya Nebraska, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani, akihubiri wakati wa ibada ya kufungua mkutano wa maaskofu wa KKKT na wa Kanisa la Marekani.



Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, alifungua Mkutano wa viongozi wa Kanisa ya Kiinjili la Kilutheri Marekani na wa KKKT. Pichani ni walioshiriki kuongoza Ibada ya ufunguzi mnamo 6 Agosti 2018.




Mch. Dkt. Wyvetta Bullock, Msaidizi wa Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani, akifurahia zawadi iliyotolewa na Mkuu wa Kanisa, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, kwa niaba ya KKKT kwenda Kanisa hilo la Marekani.



Pichani juu na hapo chini ni baadhi ya washiriki wa Mkutano wa Maaskofu wakijiandaa kwa majadiliano katika vikundi.





Askofu Dkt. Alex Mkumbo akiongoza sala ya asubuhi wakati wa mkutano wa maaskofu wa KKKT na Marekani.

Picha zote na Askofu Mike Girlinghouse, ELCA

# EKUMENE: Papa Francis afanya ziara WCC

**Na Elizabeth Lobulu**

Historia iliwekwa tarehe 21 Juni 2018 Baba Mtakatifu Francis, alipotembelea Baraza la Makanisa Duniani (WCC) jijini Geneva, Uswisi wakati wa kilele cha kumbukumbu ya miaka 70 ya WCC. Ziara hiyo ya hija iliandaliwa chini ya kauli mbiu: ***"Kutembea, kuomba na kufanya kazi pamoja."***

Kiongozi huyo wa Kanisa Katoliki duniani alisema: "Kutokuwa na umoja ni kinyume cha matakwa ya Kristo na ni kashfa inayokinzana na wito mtakatifu wa kuhubiri Injili kwa kila kiumbe.

"Kuishi imani ya Kikristo kunataka uache ubinafsi ili ujitoe kwa Yesu kwa nguvu zote. Waraka kwa Wagalatia utufundishe kuwa maisha ya kikristo ni kujitoa ukitambua ubaguzi wowote hauna nafasi kubwa katika utambulisho wetu. Unafundisha kutokuwa na ubaguzi kwa kuchagua kuwa mali ya Yesu kabla ya kuwa wa Apollo au Kefa; kuwa mali ya Yesu kabla ya kuwa Myahudi au Mgiriki; kuwa mali ya Yesu kabla ya kujitambulisha upande wa kulia au kushoto kisiasa. Hilo la kuchagua kwa kuongozwa na Injili; kuchagua wengine badala ya kujipendelea binafsi... katika macho ya dunia, linaonekana ni hasara.

"Tofauti zetu zisiwe kisingizio cha kutoshirikiana kwa kuwa hata sasa tunaweza kutembea pamoja katika Roho tukisali, kueneza Injili na kuhudumia watu kwa pamoja," Papa Francis alisema.



**Papa Francis alihutubia viongozi wa dini wakiwemo wajumbe 150 wa Kamati Kuu ya WCC alipofanya ziara Baraza la Makanisa Duniani (WCC), Geneva, Uswisi.** (Picha zote na Albin Hillert/ WCC)

Katibu Mkuu wa WCC, Mch. Dkt. Olav Fykse Tveit, alisema awali: "Ujio wa Baba Mtakatifu Francis wakati wa maadhimisho ya miaka 70 ya WCC ni alama ya kumbukumbu kihistoria ya kuuendea umoja wa wakristo na jitihada za kutafuta na kujenga ushirikiano wa makanisa ili amani na haki duniani iwepo.

"Kuanzia ngazi ya chini hadi ya kimataifa, mahusiano hayatabaki kama zamani baada ya ziara hii kwani imedhihirisha tunaweza kufanya mengi tukiwa pamoja."



**Papa Francis akifurahia zawadi aliyopewa naKatibu Mkuu wa WCC Mchg. Dkt, Olav Fykse Tveit.**

Pia Dkt. Tveit aliyaalika makanisa yote yashirikiane zaidi ili kusaidia wakimbizi, watu walioathirika na mabadiliko ya tabia nchi, walio vitani na wanaopigania haki kwa kuwekwa pembezoni.



**Papa Francis akiagana na Dkt. Agnes Abuom, Mwenyekiti wa Vikao vya Kamati Kuu WCC na Katibu Mkuu wa WCC, Mch. Dkt. Olav Fykse Tveit baada ya ziara ya siku moja WCC.**

WCC ina makanisa wanachama 348. Wanachama wanatoka madhehebu na makanisa ya nchi na maeneo 120 duniani ikiwakilisha wakristo zaidi ya milioni 560. Makanisa hayo ni pamoja na ya Orthodox, Anglikana, Baptisti, Kilutheri, Methodisti, makanisa ya *Reform* na yanayojitegemea.

Kanisa Katoliki siyo mwanachama wa WCC, lakini lina ujumbe wa kudumu katika Kamisheni ya WCC ya *Imani na Ushirika (Faith and Order)* na linashirikiana na WCC kupitia taasisi nyingine likiwemo Baraza la Kipapa linalohamasisha Umoja wa Kikristo Duniani (PCPCU). Ratiba ya Papa ilikuwa ifuatavyo: Baada ya kufika uwanja wa ndege wa Geneva kutoka Roma, Italia alikwenda kumsalimu Rais wa Uswisi, Mheshimiwa Alain Berset, na kisha kujiunga wenyeji wake, WCC.



**Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya WCC, Dkt. Agnes Agboum, akiwa jukwaani na viongozi wengine wa WCC. Papa Francis alitoa baraka katika ibada ya maombi kiekumene alipofanya ziara WCC. Kulia kwa Papa ni Katibu Mkuu wa WCC, Dkt. Olav Fykse Tveit, akifuatiwa na Askofu Mary Ann Swenson, Makamu Mwenyekiti wa Vikao vya Kamati Kuu, WCC.**

Awamu ya kwanza ilikuwa ni kutembelea Chuo Kikuu cha Kiekumene cha WCC cha Bogis-Bossey, nje kidogo ya jiji la Geneva. Wakati huo pia ulitumika kubadilishana zawadi na kula chakula cha mchana na viongozi wa WCC.

Awamu ya pili ilikuwa ibada ya kiekumene Ofisi Kuu ya WCC ambapo Papa alikutana kusalimiana na viongozi wa dini waliofika kuonna kuwahutubia viongozi wa dini wakiwemo wajumbe 150 wa Kamati Kuu ya WCC.

Kabla ya kurudi Roma, aliongoza Ibada ya misa katika Kituo cha Mikutano Palexpo.

# Mkutano wa kimataifa wa Walutheri wenye asili ya Afrika wafanyika




**Mkutano wa kwanza wa kimataifa wa Walutheri wenye asili ya Afrika (IALC) ulifanyika 9 - 13 Agosti 2018 katika Hotel ya Uhuru mjini Moshi, Kilimanjaro. Mkutano huo ulihudhuriwa na washiriki kutoka Marekani na Tanzania. Viongozi wa KKKT walikuwa ni miongoni mwa washiriki 95 waliohudhuria.**




**Baadhi ya viongozi hasa kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani wenye asili ya Afrika waliohusika kuandaa Mkutano wa IALC. Kutoka kulia ni Mch. Dkt. Emmanuel Grantson, Mwenyekiti wa IALC; Mch. Perucy Butiku, Msaidizi wa Askofu Sinodi ya Metro New York; Mch. Dkt. Joseph M. Bocko, Mratibu wa IALC na Mch. Dkt. Andrea Walker, Mkurugenzi wa Misioni ya Dunia na wote hao ni watumishi wa Kanisa hilo la Marekani. Wengine ni Mch. Dkt. Elieshi Mungure, kutoka Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani akifuatiwa na Bibi Toromare Mananato kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la Madagaska.**



**Wajumbe wa Mkutano walipohudhuria ibada Usharika wa Kathedrali ya KKKT, mjini Moshi, tarehe 12 Agosti, 2018.**



**Mchg. Dkt. Fidon Mwombeki, Katibu Mkuu wa Baraza la Makanisa Afrika (AACC) akitoa mada katika Mkutano wa Kwanza wa Kimataifa wa Walutheri wanaoishi ugenini hususan Marekani uliofanyika Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro 9-13 Agosti.**

Picha zote na
Jerome Killeo, KKKT DK



**Mch. Dkt. Albert Starr wa Marekani akitoa maoni wakati wa mkutano.**





Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, akikabidhi vyeti kwa vijana waliohudhuria Kongamano lao jijini Mwanza. Kongamano lilitanguliwa na Mkutano wa Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu wa Vijana. Watatu kulia ni Askofu Andrew Gulle wa Dayosisi ya Mashariki ya Ziwa Victoria.

# Kongamano na mkutano mkuu wa vijana vyafanyika Mwanza

Kongamano la Tano na Mkutano Mkuu wa Tatu wa Vijana wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) ulifanyikia, Shule ya Kassa jijini Mwanza 20 - 25 Juni 2018.

Kongamano hilo liliokutanisha watu 1,000 toka Dayosisi 25 za KKKT na maeneo ya misioni uliongozwa na Kauli mbiu: "Wajibu wa Kijana Mkristo na Matengenezo ya Kanisa." Neno kuu lilikuwa: ***"Tazama, sisi tumeviacha vitu vyetu vyote na kukufuata" (Lk 18: 28b).***



Baadhi ya vijana 1,000 walioshiriki Kongamano la Vijana wa KKKT lililofanyika Shinyanga.

# Mkuu aonya wanawake wasiwe na ukatili kwa wengine

Mkutano Mkuu wa 17 wa Wanawake wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ulifanyika Shinyanga 16 - 19 Juni 2018. Mkurugenzi wa Wanawake KKKT, Bibi Faustina Nillan, alisema kauli mbiu ya Mkutano huo ilikuwa: ***"Nimeona mateso ya watu wangu.... nimesikia kuugua kwao, nami nimeshuka niwatoe"*** (Mdo. 7: 34).

Washiriki wapatao 150 walihudhuria. Miongoni mwa matukio muhimu wakati wa mkutano ulikuwa uzinduzi wa **Mpango wa Usawa na Haki ya Jinsia 2018 - 2020.** Wakati wa uzinduzi huo Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, alisema wanawake huonekana wako mstari wa mbele kupigani haki za wanawake na watoto lakini baadhi yao wanafanya ukatili kwa watu wengine hasa watoto, nk. Hivyo alitaka walio na tabia hiyo waache.

# KINAPATIKANA:

## "Tumwabudu Mungu Wetu"




Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo, akizindua Kitabu kipya cha 'Tumwabudu Mungu Wetu' hivi karibuni. Wengine ni Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa (kulia) na Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala, Bw. Loata Mungaya Laizer.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) linapenda kuwatangazia Washarika wote kwamba toleo jipya la kitabu cha:

**"Tumwabudu Mungu Wetu"**

chenye umbo dogo na mwonekano mpya, kinapatikana sasa.

Bei ya nakala moja ni **Sh. 12,000/-**




### Mawasiliano:

Bi Evaline Kivo
Ofisi ya Hazina KKKT
**Simu:** +255 658 889 734
Robinson Lukumay
Ofisi ya Hazina KKKT
**Simu:** +255 783 450 791

### Kwa maelezo zaidi:

Mchg. Lazaro Rohho
NKM Misioni na Uinjilisti KKKT
**Simu:** +255 766 288 887